

JINA LA MTAHINIWA:
MKOA:

SHULE:
WILAYA:

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA



MTIHANI WA KWANZA WA UPIMAJI - FEBRUARI 2025 KISWAHILI – DARASA LA NNE

Muda: Saa1:30

Mwaka: 2025

SEHEMU A: IMLA

1. Sikiliza kwa makini sentensi utakazosomewa na msimamizi kisha uziandike kwa usahihi

- i. _____
- ii. _____
- iii. _____
- iv. _____
- v. _____

SEHEMU B: MATUMIZI YA LUGHA

2. Chagua herufi ya jibu sahihi na uiandike katika mabano.

- i. Mwalimu alitupa orodha ya maneno haya "**mahindi, mtama, uwele, ulezi**" kisha akatwambia tuandike neno moja linalojumuisha maneno yote. Unadhani tuliandika jibu gani?
A: vyakula B: madini C: nafaka D: vinywaji []
- ii. Katika mahafali ya darasa la sabaalimkaribisha Mwalimu Mkuu ili atambulisha wageni. Ni neno gani linafaa kukamilisha tungo hiyo?
A: mwalimu B: mwanafunzi C: Mgeni Rasmi D: mshereheshaji []
- iii. Unaweza kuunda tendo gani kutokana na jina hili? **Kilimo.**
A: Lima B: Limo C: Mlimaji D: Mkulima []
- iv. Upi ni ukanushi sahihi wa sentensi hii? "Mama analima kama trekta"
A: Mama alimi kama trekta B: Mama hatalima kama trekta
C: Mama halimi kama trekta D: Mama hajalima kama trekta []
- v. Ikiwa kinyume cha bondeni ni mlimani. Je, kinyume cha zamani ni kipi?
A: kale B: wahenga C: kesho D: sasa []

JINA LA MTAHINIWA:
MKOA:

SHULE:
WILAYA:

SEHEMU C: NAHAU METHALI NA VITENDAWILI

3. Oanisha Sehemu A na B kwa kuandika jibu sahihi katika sehemu ya majibu.

Sehemu A	Majibu	Sehemu B
i. Unga mkono		A: Hukosa yote
ii. Tia chumvi		B: Mlango
iii. Mtaka yote kwa pupa		C: Humaliza buyu la asali
iv. Chovya chovya		D: Kobe
v. Kila mtu humwabudu apitapo		E: Kubaliana na jambo
		F: Hapati chochote
		G: Ongeza maneno yasiyo ya kweli

SEHEMU D: UTUNGAJI

4. Tumia jedwali hapa chini kuunda maneno katika jedwali i – v.

1	2	3	4	5	6	7	8	9	10	11	12	13	14	15	16	17	18	19	20	21	22	23	24
A	B	CH	D	E	F	G	H	I	J	K	L	M	N	O	P	R	S	T	U	V	W	Y	Z

i.

2	20	3	15	18	1

ii.

18	8	20	12	5

iii.

13	5	24	1

iv.

11	1	12	1	13	20

v.

13	19	9	8	1	14	9

SEHEMU E: UFAHAMU

5. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali.

Leo saa tisa mchana Mwalimu Mkuu wetu alitangaza kuwa kila mwaka huwa kuna mashindano ya kutafuta wanafunzi wenye vipaji mbalimbali. Alisema kuwa siku ya kufunga shule mwaka huu ndiyo siku ya mashindano hayo. Alielekeza kuwa wanafunzi wote tuwe tayari. Alifafanua kuwa wataalamu wa kugundua vipaji kutoka Makao Makuu ya nchi, Dodoma, wamethibitisha kuja shuleni siku hiyo. Alisema, kwa kawaida, watu hao huchagua wanafunzi wenye vipaji mbalimbali kama vile kuchora, kucheza mpira, kuimba na vipaji vya sayansi. Wanafunzi ambao huchaguliwa hupewa zawadi mbalimbali. Pia serikali hufanya njia za kuendeleza vipaji vyao. Kwa hiyo, nimekueleza haya kwa sababu wewe hukuwepo shuleni leo rafiki yangu, na nakujua vile unapenda kuchora picha. Bahati alifurahi sana kupewa taarifa hiyo akamwambia rafiki yake Juma. "Haya tujiandae rafiki yangu."

Maswali

- Ni siku gani iliyotajwa na Mwalimu Mkuu kuwa ndiyo siku ya mashindano ya kutafuta vipaji?
- Jiji la Dodoma lina sifa gani katika habari uliyoisoma?
- Mbali na serikali kuviendeleza vipaji vya wanafunzi wataochaguliwa, nini kingine wanafunzi hao hukipata?
- Kwa kuzingatia majira, mfano alfajiri, asubuhi, alasiri, jioni na aduhuri. Badala ya kusema "**Saa tisa mchana**" unaweza kusemaje?
- Unafikiri mtoa taarifa hiyo ya Mwalimu Mkuu alikuwa ni nani?